# MASOMO YA MSINGI YA BIBLIA

## KWA MKRISTO MPYA ANAYEKUA

Jina: ____________________________________________________________

Anwani ____________________________ Nambari ya Simu _____________

Tarehe ya Kubadilishwa: __________________________________________

**Maelezo kwa Mshauri au Mkufunzi**

1. Bahasha hii ya kwanza inapaswa kupewa muumini mpya baada ya kuokoka.
2. Masomo saba yaliyobaki yapewe muumini huyo mpya, moja baada ya nyingine, kwa kipindi cha muda uliopangwa somo moja kila juma.
3. Wakati wa kupeleka somo la pili kwa muumini mpya, umpe pia bahasha ambayo ataweka masomo aliyokamilishwa pamoja na kadi za vifungu au mstari wa kumbukumbu za kila somo.
4. Wakati somo jipya linapeanwa, jadili pamoja na muumini juu ya somo lililotangulia. Majibu aliyoandika yatasaidia kukujulisha ni sehemu gani anazohitaji msaada zaidi au mwongozo.
5. Mwagize muumini akate kadi za mstari wa kumbukumbu katika kila bahasha kama ilivyoonyeshwa, na kwa njia yoyote ile, aitumie kumsaidia kujifunza mstari.

ILANI: Haipendekezwi kupeana masomo haya yote kwa wakati mmoja. Kufanya hivyo kunaweza kumtatiza muumini au Mkristo mpya. Kumpa somo juma-kwa-juma kutahakikisha kwamba utakutana naye kibinafsi kwa muda masomo yatakuwa yanaendelea.

**Rekodi ya Maendeleo**

| Nambari ya Somo | Tarehe Alipomaliza | Maoni/Maagizo |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |

Kimetayarishwa na Charles “Chic” Shaver, Toleo la Kiswahili limetafsiriwa na Julius Njuki,
Toleo la pili 1994 limechapishwa na Beacon Hill Press of Kansas City.
Ukitaka nakala zaidi, andika kwa Idara ya Vitabu ya Kanisa la Mnazareti
S.L.P 20025-00200 Nairobi, Kenya

# 1. NI NINI KILICHOTENDEKA KWANGU?

**Mstari wa Kumbukumbu:** Ufunuo wa Yohana 3:20

Jina……………………………...………………… Tarehe ………………….

Angalia katika Biblia yako au Agano Jipya majibu ya maswali yafuatayo. Ukiona imeandikwa hivi: Yohana 1:12, maana yake ni Injili ya Yohana, sura 1, mstari wa 12. (Orodha ya majina ya vitabu inaorodhesha nambari za kurasa.) Soma jibu kutoka katika Biblia, kisha uandike jibu hilo ukitumia maneno yako mwenyewe. I wapo una Agano Jipya peke yake umeandikiwa maandiko ya Agano la Kale katika somo hili.

1. Wakati nilimkaribisha na kumpokea Kristo nilifanyika …………. ……………………………………………......wa Mungu (Yohana 1:12)
2. Kuingia kwa Kristo katika maisha au moyo wa mtu ni uhusiano wa kibinafsi kati ya Kristo na yule anayempokea, ulioelezwa na Kristo katika Ufunuo 3:20
   a. Ni nani anayebisha mlangoni? (Angalia katika kitabu cha Ufunuo 1:1 kwa maelezo zaidi) ………………………………………………
   b. Ni nani anayeweza kuitikia sauti yake na kumfungulia mlango? …………………………………………………………………..........
   c. Ananitaka mimi nifanye nini? ……………………………………..
   d. Atafanya nini ikiwa nitafungua mlango? ……………………………. ……………………………………………………………………...
   e. Nitafungua mlango namna gani? (Tazama Ufunuo 3:19)……………. ……………………………………………………………………...
   f. Je, umefungua mlango? ……………………………………………

……………………………………………………………………………..

g. Yesu Kristo yuko wapi wakati huu? …………………………………

3. Kristo alikuja kutafuta na kutokoa kwa sababu sisi tulikuwa …………………………………………………………........…(Luka 19:10)
4. Kulingana na Warumi 3:23, hali yetu ya kupotea ilisababishwa na ukweli gani?.........................................................................................
5. Biblia inatangaza kuwa adhabu au mshahara wa dhambi ni nini (Warumi 6:23) ………………………………………………………...
6. Ni nani ambaye tayari ameshakufa kwa ajili ya dhambi zangu? Isaya 53:6 inasema "Sisi sote kama kondoo tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe, na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote." (Tazama Warumi 5:8-9 kutambua zaidi ni nani aliyetufia)…………………………………………………….............

   ……………………………………………………………………………
7. Wakati nilikiri na kutubu dhambi zangu, Mungu alifanya nini? (1 Yohana 1:9). Tofautisha kitabu cha 1 Yohana, ambacho kiko karibu na mwisho wa Agano Jipya ambacho ni moja ya barua za Yohana), na Injili ya Yohana ……………………......................................................

   ……………………………………………………………………………
8. Yanipasa kufanya nini juu ya dhambi ambazo nimetubu kwa dhati na kumwambia Mungu anisamehe? Isaya 55:7 inasema, "mtu mbaya na aache njia yake, na mtu aisye haki aacha mawazo yake na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa." Piga mstari chini ya maneno ambayo yanaonyesha vile utafanya kuhusu dhambi au njia zako mbaya).
9. Kulingana na Waefeso 2:8-9, njia ya kupokea wokovu (piga sahihi )

   ☐ a. Kutenda kazi nyingi nzuri

☐ b. Kujairub kadiri niwezavyo kutenda yaliyo mema

☐ c. Kuukubali msamaha wa Mungu kwa imani.

10. Lakini mara tunapopokea wokovu na kufanywa viumbe vipya na Kristo, kusudi la Mungu kwetu ni (Waefeso 2:10) …………….........
…………………………………………………………………
………………………………………………………………….

11. Ni nani ambaye tunamjia kwa njia ya Yesu Kristo? (Yohana 14:6, 9)
…………………………………..........................................

12. 1 Yohana 5:13 inasema kwamba wewe ambaye umeamini au umeweka imani yako kwa Yesu Kristo, mwana wa Mungu unaweza kutumaini, kufikiri, kujua (chagua jibu sahihi) kwamba una uzima wa milele……………………………………………………………...

13. Ikiwa nitakufa usiku wa leo, nitakwenda wapi? (Yohana 6:47) ……….
………………………………………………………………….

14. Eleza kwa ufupi kile kinachokufanya ujue kuwa wewe ni mtoto wa Mungu ………………………………………………………….
………………………………………………………………….

15. Sasa kwa vile nimezaliwa kiroho na kuwa mtoto wa Mungu (Yohana 3:3-7, ninahitaji chakula cha kiroho ikiwa ninataka kuishi na kukua. Ni kitu gani cha kwanza ambacho kitahitajika katika chakula change? (Mathayo 4:4) ………………………………………………….
……………………………..........................................................

**Maelezo zaidi ya kukua kiroho**

a. **Kwa hivyo soma Biblia yako kila siku.** Hicho ndicho kitu cha kwanza katika chakula chako. Tenga muda Fulani kila siku kufanya hivyo. Anza kwa kusoma Injili ya Yohana-sura moja kila siku. Kila moja la masomo haya ya Biblia litakuwa na maswali kadha kutoka

kitabu cha Yohana na vitabu vingine vya Biblia. Kata sehemu ya “aya ya kukariri” ya kila somo na utembee nayo mfukoni mwako na ujifunza kwa tafsiri kadha. Chagua moja ambayo inakufutia zaidi.

b. **Omba kila siku.** Sema na Mungu moja kwa moja kutoka moyoni mwako.
c. **Hudhuria kanisa kila wakati** milango inapokuwa wazi-kanisa ambalo Biblia inahubiriwa na Kristo anatukuzwa.
d. **Mtii Mungu.** Ikiwa hujui kama tendo Fulani ni jema ama mbaya, jiulize, “Yesu angefanya nini?”
e. **Shuhudia.** Mwambie mtu mwingine mambo ambayo Bwana amekufanyia.

Sasa unaeleza vizuri ni “Nini kilitendeka kwangu.” Hata hivyo, huu ni mwanzo tu wa maajabu makubwa yaliyotokea kwako. Kuna mengi zaidi!

**Mstari wa Kumbukumbu**

Tazama, nasimama mlangoni, nabisha: mtu akiisikia sauti yangu na kuufungua mlango, nitaingia kwake name nitakula pamoja naye, nay eye pamoja name (Ufunuo 3:20)

# 2. KUTEMBEA NA MUNGU

**Mstari wa Kumbukumbu:** 1 Wakorintho 10:13

Jina ………………………………………………... Tarehe………………..

Mara mtoto anapozaliwa kimwili, anapaswa kuanza kukua. Hatua muhimu katikai kukua ni kujifunza kutembea. Hali iko vivyo hivyo hata katika maisha ya kiroho. Mtoto wa Mungu (yule ambaye amezaliwa katika Bwana) hujifunza kutembea na Mungu. Tunapoelezea maisha ya Kikristo kama "kutembea na Mungu" inaonyesha kwamba Ukristo ni uhusiano ("na Mungu"), na kwamba unaendelea ("unatembea") – haukusimama wima, na kwamba ni kukua halisi, hatua moja kwa wakati mmoja, Mtume Mika aliorodhesha kama mojawapo ya matakwa muhimu ya mwanadamu "kutembea kwa unyenyekevu na Mungu" (Mika 6:8)

1. Ulipoanza kusoma Injili ya Yohana, unaweza kuwa umetambua maelezo kadha tofauti ambayo yetumiwa katika Yohana yenye maana sawa na kutembea na Mungu. Baadhi ya maelezo hayo ni yapi?
   a. Yohana 8:12 ……………………………………………………….
   b. Yohana 1:37 ……………………………………………………….
   c. Yohana 2:5 ………………………………………………………...
   d. Yohana 5:14 ……………………………………………………….
2. Ni nani anayepinga kutembea kwetu na Mungu (1 Petro 5:8)

   ….……………………………………………………………………..
3. Shetani alifanya nini katika Mathayo 4:1? ………………………………
4. Je, Yesu alishindwa na majaribu? (Waebrania 4:15) ……………………

   Majaribu na dhambi ni sawa? ………………………………………

   (Majaribu husema "je utafanya?" dhambi husema "nitafanya!")
5. Tunapaswa kufanya nini shetani akatushambulia? (Yakobo 4:7)

…………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………..

6. Kwa maneno yako mwenyewe: Dhambi ni nini? (Angalia 1 Yohana 3:4 na Yakobo 4:17) ………………………………………………………… …………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………..

7. Isaya 59:2 inasema, "Lakini maovu yenu yamewafarakanisha nyinyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hawezi kusikia." Jambo la pekee linaloweza kunitenganisha na Mungu ni …………………………………………………………………………

8. Je, Mkristo kwa nguvu ya Kristo, anaweza kuacha kutenda dhambi makusudi? (1 Yohana 3:9) ………………………………………………

9. Ahadi ya Mungu kwetu ni nini wakati tunajaribiwa? (1 Wakorintho 10:13) Atatutengenezea-Hatatutengenezea (chagua neno sahihi) njia ya kuepuka au kuvumilia majaribu. ………………………………………...

10. Ni nini mathumuni ya maandiko ya YOhana kama ilivyoelezwa katika 1 Yohana 2:1 ……………………………………………………………… …………………………………………………………………………… ……………………………………………………………………………

11. Hata hivyo iwapo Mkristo ataanguka katika dhambi, kulingana na 1 Yohana 2:1 anapaswa (chagua jibu sahihi):
    a. – Kusema hawezi kuepuka ila kutenda dhambi
    b. – Kuficha dhambi zake na kujifanya kama kwamba hakuzitenda
    c. – Kumwendea Yesu mara moja na kutubu dhambi na kuendelea kumwishia Mungu.

d. – Kukata tama na kusema kuwa hakuna haja ya kuishi maisha ya Kikristo

12. Ikiwa Mkristo ametenda dhambi na kutubu dhambi hiyo Mungu atafanya nini? (1 Yohana 1:9) ………………………………………………..

13. Kulingana na Yohana 14:21, kutii amri za Kristo kunathibitisha nini? ……………………………………………………………………………

14. Kulingana na Yohana 10:27-29,

   a. Ni nani aliye na uzima wa milele na anayelindwa na nguvu za Mungu?

      …………………………………………………………………….

   b. Kuwa kondoo wa Kristo (mstari wa 27) ni lazima nisikie sauti ya Kristo, ijulikane naye, na …………………………………………

Hapa kuna shauri la busara na linalohitajika: Tembea na Mungu! Hiyo ina maana ya kupinga majaribu, kumtii Mungu, kumfuata Kristo. Mafundisho zaidi ya jinsi ya kufanikiwa maishani na kukua kiroho yanapatikana katika somo litakalofuata.

**Mstari wa Kumbukumbu**

Jaribu halikuwapata nyinyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu, ila Mungu ni mwaminifu ambaye hatawaacha mjaribiwe kuptia awezavyo, lakini pamoja na lile jaribu, mlango wa kutokea ili uweze kustahimili. (1 Wakorintho 10:13)

# 3. KUJIFUNZA KUTOKA KWA MUNGU

**Mstari wa Kumbukumbu: Zaburi 119:11**

Jina ………………………………………………. Tarehe ………………….

Ikiwa ungegundua kwamba mipango ya Mungu kwa ulimwengu na kwako binafsi ilikuwa imeandikwa katika kitabu, kitabu hicho kingekuwa cha thamani gani kwako? Ikiwa ahadi za Mungu kwako nay ale Mungu anayotarajia kwako yameandikwa katika kitabu, na wewe unakitabu hicho, utatumia muda gani ukisoma hicho kitabu? Kwa dakika chache zinazofuata, unaweza kufanya uvumbuzi wa ajabu!

1. Ni kitu gani kinachosemwa kuhusu neno la Mungu katika Yohana 17:17?

   Neno la Mungu ni ……………………………………………..
2. Maandiko yaliletwaje kwetu ili tuwe na uhakika wa ukweli huo? (2 Timotheo 3:16) ……………………………………………………….

   ………………………………………………………………………
3. Ni kitu gani ambacho neno la Mungu (ujumbe au amri) litafanya kwetu kulingana na:

a. 2 Timotheo 3:15? ………………………………………………..
b. Yohana 15:3? ………………………………………………………
c. Matendo ya Mitume 20:32? ………………………………………

4. Wakati ulikuwa ukisoma Injili ya Yohana, umeona mafundisho juu ya umuhimu wa Neno?

a. Kristo alifanya nini na Neno la (amri au asemavyo) Baba yake? (Yohana 8:55) …………………………………………………………

b. Neno la Mungu (ujumbe au ukweli) lina nafasi gani katika maisha ya watu wengine? (Yohana 8:37) ……………………………………………..

c. Kama sisi ni “wa Mungu au ni mali ya Mungu, tunafanya nini kuhusu Neno lake (Yohana 8:47) ……………………………………………………..

d. Ni kitu gani ambacho mwanafunzi halisi wa Kristo atafanya na neno lake (ufunuo au Mafundisho)? (Yohana 8:31) …………………………..

…………………………………………………………………………

e. Tunafanya nini na neno (amri, fundisho, au asemavyo) ili tudumishe uzima wa kiroho na wa milele? (Yohana 8:31) …………………………

…………………………………………………………………………

5. Ikiwa nampenda Kristo, nitafanya nini? (Yohana 14:23) ……………….

…………………………………………………………………………

6. Neno liliandikwa linanielekeza kwa mtu gani? ……………………… ili niweza kupata kipawa gani? ……………………………………. (Yohana 20:31)

7. Shetani anaweza kujaribu kupigana nasi katika maisha yetu ya Kikristo, lakini Mungu ametupa silaha ambayo inaweza kumshinda shetani. Silaha hiyo ni upanga wa Roho ambao ni ………………………. ………….……………………………………………(Waefeso 6:17)

8. Yesu alimshinda shetani kwa njia gani katika Mathayo 4:4, 7, 10?

…………………………………………………………………………

9. Nitafanya nini na Neno la Mungu ili nijiepushe na kutenda dhambi kinyume chake, kulingana na Zaburi 119:11 inayosema: “Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi?”…………………………………………………………

……………………………………………………………………………...

10. Ni ukweli gani kutoka katika neno la Mungu ambao hasa umekusaidia hivi karibuni?..............……………………………………………………..

………………………………………………………………………………

11. Kwa nini Mkristo anapaswa kusoma Biblia kila siku? …………………

………………………………………………………………………………

Zaidi ya “kujiufnza kutoka kwa Mungu” una thawabu nyingine ya ajabu sana kama Mkristo. Imefichuliwa katika somo litakalofuata.

**Mstari wa Kumbukumbu**

Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi. (Zaburi 119:11)

# 4. KUZUNGUMZA NA MUNGU

**Mstari wa Kumbukumbu: Yohana 16:24**

Jina…………………………………………………….. Tarehe ………………..

Maadam tunajishughulisha na Mwenyezi Mungu, si jambo kubwa kutarajia kwamba tunampa Yeye sehemu kubwa ya kila siku. (Kwa wengi wetu hii itamaanisha mapema asubuhi.) Wakati wowote ule, mahali faraghani, nasema Naye, na Yeye anazungumza nami. Mwandishi wa Zaburi alisema hivi: "Bwana asubuhi utaisikia sauti yangu; asubuhi nitaelekeza dua yangu kwako na kutazamia" (Zaburi 5:3). Hebu tuangalie ni ushauri gani zaidi ambao Biblia inatupatia kuhusu safari ya maombi.

1. Je, Yesu aliamini juu ya kuwa na wakati wa faragha wa maombi na Baba yake? (Marko 1:35) ……………………………………………..
2. Ni wakati gani ambao ninapaswa kusali? (Luka 18:1) ………………….

   ………………………………………………………………………
3. Ni nia au hali gani ambayo ni lazima iwe sehemu ya kila sala? (1 Wathesalonike 5:17-18) ……………………..…………………………..
4. Ni kitu gani kikubwa ambacho husababisha maombi kutojibiwa? "Ikiwa nitaona au kuwaza maovu moyoni mwangu, Bwana hatanisikiliza." (Zaburi 66:18) ……………………………………………………...
5. Ni kitu gani ambacho kitaamua yale tunayoomba? (Yohana 5:14). ………………………………………………………………………
6. Ni mafundisho gani ambayo umejifunza kutoka katika Injili ya Yohana kuhusu maombi? ……………………………………………………...
   a. Ni haki gani ambayo kila Mkristo anayo? (Yohana 16:24) ……………………………………………………………………...

      …………………………………………………………………......

b. Kusudi la Mungu katika kujibu maombi ni kwamba ………………
………………………………………………………… (Yohana 14:13)

c. Ni jambo gani ambalo Kristo anataka kwetu ili ajibu maombi yetu? (Yohana 15:7) ……………………………………………………..
……………………………………………………………………...

7. Ili niweze kupata jibu, ninapaswa kufanya nini wakati ninasali? (Mathayo 21:22) ………………………………………………………

8. Baadhi ya maombi maalum, ambayo ninaweza kuomba ni:

a. Mathayo 6:11 ……………………………..……………………….

b. Mathayo 9:38 ……………………………..……………………….

c. Wafilipi 1:9 ……………………………..…………………………

d. 1 Timotheo 2:1-2……………………………………………….

e. Yakobo 1:5 ……………………………………………………….

9. Ni kitu gani ambacho kinaweza kunizuia nisiingie majaribuni? (Mathayo 26:41) ………………………………………………………
……………………………………………………………………

10. Sala nzuri zaidi ni zile ambazo (Chagua jibu sahihi):

.................... a. hutumia maneno yanayofaa ya dini

…………… b. "zinasikika kama maombi"

……………. c. zinatoka moyoni mwangu

11. Una mipango gani juu ya muda wa maombi yako faragha na Bwana?
…………………………………………………………………
…………………………………………………………………
…………………………………………………………………

Pengine hutakumbuka jinsi ilivyo kubwa thawabu na haki yako katika kusema na Mwenyezi Mungu. Upengo na Baraka zote ambazo

amekuonyesha zinasababisha wewe kumtumikia, sivyo? Kwa hivyo jifunze somo litakalofuata.

**Mstari ya Kumbukumbu**

Hadi sasa hamjaomba chochote kwa jina langu. Ombeni nanyi mtapata, ili furaha yenu iwe timilifu. (Yohana 16:24)

# 5. KUSHIRIKI NA MUNGU

**Mstari wa Kumbukumbu: 1 Wakorintho 10:31**

Jina. ……………………………………….. Tarehe ……………………..

Ikiwa ninaamini kweli juu ya kitu fulani, nitakitegemeza kikamilifu, kwa asilimia 100. Na sasa Mungu ninakuamini kabisa zaidi sana kuliko mwanzo! Kwa hivyo ninataka kukupendeza, kukutumikia na kushiriki nawe vile nilivyo na kwa vyote nilivyo navyo.

Mtume Paulo alieleza jambo hilo hivi: “Basi mlapo au mnywapo au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu” (1 Wakorintho 10:31). Katika mambo makubwa au mambo madogo, kaktika kila jambo ninalofanya nitajiuliza, “jambo hili linamtukuza Mungu?”

1. Kulingana na Mathayo 22:36-40
   a. Ninapaswa kumpenda Mungu kiasi gani? …………………………...
   b. Ninapaswa kumpenda jirani yangu kiasi gani? ………………………
2. Nitaonyeshaje upendo kwa Mungu na watu wengine? (Yohana 5:2-3) ……………………………………………………………………………
3. Yohana alikuwa na yapi ya kusema kuhusu kujitoa kikamilifu kwa Mungu nay ale yampendezayo?
   a. Ili punje ya ngano iweze kuzaa mavuno mengi, ni lazima ifanye nini? (Yohana 12:25-25) ..…………………………………………...
   b. Ikiwa nitamtumikia Yesu Kristo badala ya ambo yangu binafsi, Baba atafanya nini? (Yohana 12:26) ………………………………………
4. Sasa kama Mkristo nina nia mpya katika uhusiano wowote nilio nao maishani, kwa sababu ya uhusiano wangu mpya na Mungu. Ninapokuwa

“katika Kristo” (Mkristo aliyeungana na yeye), Mambo ya kala yamepita? (2 Wakorintho 5:17) …………………………………….

. ……………………………………………………………………..

a. Uhusiano wangu mpya kwa mambo mbali mbali:

(1) Sasa nintaka kutoa/kujiweka. (chagua neno sahihi) (Luka 6:38)

(2) Chagua mambo matatu yaliyo sawa yaliyotajwa katika Waefeso 4:28

(a) Kuacha kuendelea kuiba

(b) Kuwa mfanyi kazi mwenye bidii

(c) Kujiwekea yote kwangu

(d) Kushiriki nilivyo navyo na wahitaji

(e) Kuiba kama inawezekana

(f) Kukaa bila kufanya kazi yoyote.

(g) Uhusiano wangu mpya kwa watu wengine:

b. Uhusiano wangu mpya kwa watu wengine:

(1) Nitakuwa ……………………………………………………….. ………………………………… kwa watu wengine. (Waefeso 4:32)

(2) Ninapaswa kuepuka, kutafuta (chagua neno sahihi) kushirikaina na watu wasioamini, ili niweze kutumikia haki kikamilifu (2 Wakorintho 6:14)

c. Uhusiano wangu mpya kwa nafsi yangu:

(1) Katika kujifunza jinsi ninavyoonekana na matumizi ya mwili wangu, ni lazima nikumbuke kwamba Mwili ni hekalu la ………………… (1 Wakorintho 6:19)

(2) Ninapaswa ……………………………………… wakati wangu na nafasi niliyo nayo (Waefeso 5:16)

5. Ninapaswa kupenda …………………………… (1 Yohana 2:10), lakini sipaswi kupenda ………………………………….. (1 Yohana 2:15-16)

6. Kwa nini Mungu anatutarajia tumtukuze Yeye? (! Wakorintho 6:20)

   ……………………………………………………………………………

7. Ikiwa nitaweka ufalme wa Mungu na haki Yake. (uadilifu au utakatifu) kwanza, matokeo yatakuwa nini? (Mathayo 6:31-33)

   ……………………………………………………………………………

8. Tunaposhiriki na Mungu maisha yetu yote, kwa kuitikia upendo wa Mungu kwetu, ni nani anayefaidika zaidi? (Marko 10:28-30)

   ……………………………………………………………………………

9. Ili niweze kushiriki kikamilifu na Mungu, nitafanya haya: ……………..

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

Ukweli huu utafunuga njia ya kutuwezesha kufikia furaha ya sisi kujishirikisha na Mungu. Tena kuna aina nyingine maalum ya ushirika tunayofanya wakati tunazungumza kuhusu Kristo kwa wengine. Inaitwa ushuhuda, na somo litakalofuata linazungumzia jambo hilo.

**Mstari wa Kumbukumbu**

Basi mlapo au mnywapo au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu (1 Wakorintho 10:31)

# 6. KUZUNGUMZA KWA NIABA YA MUNGU

**Mstari wa Kumbukumbu: Mathayo 4:19**

Jina……………………………………………. Tarehe ……………………

Fikiria umekutana na rafiki yako wa zamani ambaye afya yake ilikuwa mbaya sana kiasi kwamba mara ya mwisho ulipomwona hukutarajia kuwa ataendelea kuishi. Sasa anaonekana mwenye afya njema. Anadai kwamba amepata daktari ambaye amemponya. Lakini huyo rafiki yako hatakai kusema jina wala anwani ya daktari huyo. Labada wewe unasema moyoni, "haiwezekani kwa rafiki kufanya hivyo!" Ni watu wangapi ambao wameponywa kabisa kiroho na Kristo na wanapuuza kuwaambia wengine jinsi wanavyoweza kuponywa! Kushuhudia ni kuwaambia wengine yale ambayo Kristo amekufanyia.

1. Uponyaji wa Kristo kwa yule mwenye pepo ulifuatiwa na amri dhahiri. Ni ufafanuzi gani wa neno "kushuhudia" unaupata hapa? (Luka 8:39)

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

2. Injili ya Yohana inatufundisha mambo mengi juu ya kushuhudia.

a. Kulingana na Yohana 3:32 kushuhudia (au kutoa ushahidi)ni kushiriki na wengine (chagua jibu sahihi hapa chini)

   ☐ (1) Yale uliyofundishwa kuwa ni ukweli

   ☐ (2) Yale ambayo umesikia kutoka kwa watu wengine

   ☐ (3) Yale ambayo umeyaona na kusikia (ambayo una ujuzi nayo).

b. Andrea alikuwa anfanya nini katika Yohana 1:40-41? …………………

   ……………………………………………………………………………

c. Yesu alisema ni kazi gani muhimu zaidi ya Mungu kwa Mkristo kufanya (Yohana 6:28-29) ………………………………………………

…………………………………………………………………………………

d. Ni kazi gani anayotuambia tufanye katika Yohana 15:16? ……………...

…………………………………………………………………………………

3. Ni kitu gani cha muhimu zaidi ambacho kimewahi kutendeka kwako?

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

4. Ukarimu mkubwa ambao ninaweza kumfanyia mtu mwingine ni:

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

5. Yesu anatuamuru tufanye nini katika Mathayo 28:18-19? ……………...

…………………………………………………………………………………

6. Ni tukio gani ambalo Wakristo wa kwanza walishiriki kama thibitisho kwamba walikuwa wamemkubali Kristo? (Matendo ya Mitume 8:12, 35-38) …………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

Je, umeshafanya jambo hili kama dhihirisho la imani yako? (Chagua jibu moja hapa chini).

☐Ndio ☐Hapana ☐Nafikiria kuhusu jambo hilo.

7. Hali ya wale wasioamini katika Kristo ikoaje? (Yohana 3:18) …………

…………………………………………………………………………………

8. Ikiwa mimi ni mwaminifu katika kumfuata Kristo, yeye ameahidi (Mathayo 4:19) ……………………………………………………….

……………………...…………………………………………………….

9. Kulingana na 1 Petro 3:15, ninaweza kujitayarisha kumshuhudia Kristo kwa wengine kwa ……………………………………………………….
…………………………………………………………………………
10. Paulo alikutana na watu wapi ili awajulishe habari za Kristo? (Matendo ya Mitume 17:17, 20:20) ………………………………………………..
…………………………………………………………………………
11. Kwa nini kiini cha ushuhuda wetu lazima kiwe Kristo? (Yohana 14:6)
…………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
12. Kama mashahidi wa Kristo, ujumbe wetu kwa wale wasio na Kristo unapaswa kuwa nini?

Warumi 16:23 …………………………………………………………

Warumi 3:23…………………………………………………………..

Isaya 53:6 – "sisi sote kama kondoo tumepotea …… na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote" ………………………………..

…………………………………………………………(Yohana 1:12)

13. Baada ya mtu kumkubali Kristo, wajibu wetu kwake ni nini? (Matendo ya Mitume 14:21-22) ……………………………………………………….

14. Ushahidi au ushuhuda unaofaa una sehemu tatu: (1) Vile nilivyokuwa kabla sijawa Mkristo; (2) Jinsi nilivyokuwa Mkristo; (3) Kristo ameleta mabadiliko gani katika maisha yangu. Andika ushuhuda mfupi ambao unaweza kumshuhudia rafiki yako.

    ……………………………………………………………………………

    ……………………………………………………………………………

    ……………………………………………………………………………

    ……………………………………………………………………………

15. Andika majina ya watu watatu ambao unajua wanamhitaji Kristo na ambao utawaombea na kuwashuhudia wakati nafasi itakapatikana.

    1. . …………………………………………………………………..
    2. ……………………………………………………………………
    3. ……………………………………………………………………

Lakini ingawa unajua ni lazima uwaambie wengine kuhusu Yesu Kristo, unaweza kuogopa kufanya hivyo. Utapata wapi nguvu za kusema nao licha ya kuogopa? Jambo hilo ndilo litakalofunzwa katika somo litakalofuata.

**Mstari wa Kumbukumbu**
Mathayo 4:19
Akawambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu.

# 7. KUJAZWA NA ROHO WA MUNGU

**Mstari wa Kumbukumbu: Waefeso 5:18**

Jina …………………………………………………Tarehe ………………….

Ni mara ngapi Mkristo anasema, "nintaka kumtumika Mungu zaidi lakin sina uwezo wa kufanya hivyo?" Kuna jibu moja tu kwa tatizo hili. Mkristo ni lazima awe na nguvu zaidi za Mungu kupitia kwa Roho anayeishi ndani yake. Hii ndio sababu Paulo aliwaambia Wakristo wa wakati wake, "Jazweni na Roho" (Waefeso 5:18)

1. Yesu Kristo alitumia wakati mwingi akiwafundisha wanafuzni wake kuhusu Roho Mtakatifu na Yoyaha ameandika baadhi ya mafundisho hayo kwa ajili yetu.
    a. Ni nani ambaye Yesu alisema atatupa ujuzi uanofurika kwa Mungu. (kama mino ya maji ya uzima)? (Yohana 7:38-39) ………………….
    ……………….……………………………………………………….
    b. Ni nani atakayetufundisha? (Yohana 14:26) …………………………
    c. Ni nani "anayeshuhudiwa" na Roho Mtakatifu wa ukweli, yaani Roho Mtakatifu huwa anashuhduia au kusema kuhusu nani? (Yohana 15:26) ……………………………………………………………………...
    d. Ni wakati gani katika maisha ya Mkristo ambao Roho Mtakatifu huanza kufanya kazi. (Yohana 3:5) …………………………………
2. Ni kutoka kwa nani wanafunzi wa Kristo bado walihitaji kupta nguvu za kuwawezesha kushuhudia (Matendo ya Mitume 1:8) …..........................
    ……………………………………………………………………………

3. Je, Paulo alihitaji nini kiroho, hata kama alikuwa tayari amemkubali Kristo? (Matendo ya Mitume 9:17) …………………………………...
4. Mambo yanayomzuia mtu kuwa wa kiroho au kuwa mtu aliyejazwa na roho yameonyeshwa katika kanisa la Korintho. Walionyesha nia mbaya kama vile wivu, ambayo ilidhihirisha walikuwa bado …………………..
…………………………………………………………………………
5. Je, ni kazi gani maalum ambayo Roho Mtakatifu hufanya ambayo inaota vizuizi kwa milki Yake timilifu na kutufanya kuwa wasafi, au watakatifu, na kututenga kwa ajili ya Mungu? (1 Petro 1:2) ……………
…………………………………………………………………………
6. Je, Yesu aliwaombea wanafunzi wake jambo gani? (Yohana 17:17) …...
….…………………………………………………………………...
7. Wakati Mungu aliwapa Kanisa la kwanza utimilifu wa Roho Mtakatifu, je, alifanya nini kuhusu uchagu au kutokuwa wasafi katika mioyo yao? (Matendo ya Mitume 15:8-9) ………………………………………
8. Je, tunapaswa kufanya nini na nia yoyote iliyo chafu au yenye dhambi katika maisha yetu? (2 Wakorintho 7:1) ………………………………..
……………………………………………………………………..
9. Je, Mungu hutaka kukumilika huku kwa utakaso (kusafishwa au utakaso) kuwe kwa kiwango gani? (1 Wathesalonike 5:23) …………….
…………………………………………………………………….....
10. Je, nani atakayenitakasa kabisa? (1 Wathesalonike 5:23) ………………
…………………………………………………………………………
11. Sheria au kanuni ya ……………………………………………….. inaniweka huru kutoka kwa sheria ya dhambi na mauti. (Warumi 8:2)

12. Nia mbaya ya Wakorintho (1 Wakorintho 3:1-3) inaonyesha kwamba walikosa sifa ambayo ni ya maana sana katika maisha ya Mkristo. Ni. ………………………………….. (1 Wakorintho 13:13)
13. Ninaweza kupokea upendo (wa Mungu) kutoka kwa …………………………….. (Warumi 5:5)
14. Baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu, je ni uhusiano gani ninaostahili kuudumisha na Yeye? (Warumi 8:4) …………………………………… ……………………………………………………………………………
15. Je, uhusiano wangu wa sasa na Roho Mtakatifu uko vipi? ……………………………………………………………………………

Maisha ya Kikristo yaliyotakaswa na yenye nguvu ni yale yaliyojazwa na Roho. Yanadhihirika kwa wengine. Je, ungependa kujazwa na Roho? Kuna hatua nne rahisi:

a. Muombe Mungu akujaze na Roho katika ukamilifu wake (Luka 11:13)
b. Mpe Mungu maisha yako yote (Warumi 12:1-2)
c. Ukiri haja yako ya kutakaswa au kusafishwa ndani (Matendo ya Mitume 15:8-9)
d. Mpokee Roho atakasaye kwa tendo la imani. (Matendo ya Mitume 15:8-9; 1 Wathesalonike 5:23-24).

**Mstari wa Kumbukumbu**

Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe na Roho (Waefeso 5:18)

# 8. KUUNGANA KWA AJILI YA MUNGU

**Mstari wa Kumbukumbu: Waebrania 10:25**

Jina ……………………………………… Tarehe …………………………

Je, umetambua kwamba wakati ulimpokea Yesu Kristo, hukumpata Baba yako wa mbinguni tu, bali pia ulipata jamii mpya kabisa ya Kikristo? Kila Mkristo halisi alifanyika ndugu au dada yako. Jamii hii mpya ambayo unahusiana nayo inaitwa "kanisa". Hakika unaonyesha jamii yako ya kiroho upendo mwingi.

1. Biblia inawataja wafuasi wa Kristo kwa majina tofauti. Andika namna tatu ziliztumiwa kutja wafuasi wa Kristo katika Matendo ya Mitume 11:26.

   (a) ……………………………………………………………………...

   (b) ……………………………………………………………………...

   (c) …………………………………………………………………….

2. Kwa vile tunapaswa kufanya kazi pamoja kama Wakristo, kanisa wakati mwingine linaitwa ……………………………………………………….

   ……………………………………………………(1 Wakorintho 12:27)

3. Ni nani Kichwa cha Kanisa? (Waefeso 5:23) …………………………..

4. Ni tendo gani la Kristo linalotuonyesha jinsi kanisa lilivyo muhimu kwake? (Waefeso 5:25) ……………………………………………………

5. Ili niwe sehemu ya kanisa, ninapaswa kuwa na uhusiano gani na Kristo? (Waefeso 5:24) ……………………………………………………..........

6. Ni wapi ambapo Paulo alikuwa amefundisha njia za Kristo? (1 Wakorintho 4:17) ……………………………………………………….

7. Ni mafunzo gani ambayo Injili ya Yohana inekufunza kuhusu kanisa? ……………………………..………………………………………….

a. Ulimwengu utajua vipi kwamba mimi ni wa kanisa la kweli (la wafuasi wa Kristo)? (Yohana 13:35) ………………………………………………..

b. Wajibu wa mchungaji ni kwa kanisa? (Yohana 21:16) ………………… ……………………………………………………...................................

8. Ni kwa njia gani maalum ambayo tunamkumbuka Yesu Kristo na yale ametufanyia? (1 Wakorintho 11:23-26) ………………………………… ……………………………………………………..................................

9. Ninapaswa kumtendea namna gani mshiriki mwenzangu wa kanisa (Wagalatia 6:2) ……………………………………………………………

10. Wakati Roho Mtakatifu anawapa watu binafsi vipawa maalum, kusudi lake ni nini? (1 Wakorintho 12:4, 7) ……………………………………. ……………………………………………………...................................

11. Makanisa mengine yna nguvu na upendo na mengine hayana. Ni kanisa gani kati ya makanisa haya mawili yafuatayo ambalo ungependa kusaidia au kuwa mwanachama wake? (Chagua moja ▤)

☐ (a) Kanisa lililoko Yerusalemu (Matendo ya Mitume 4:32-33)

☐ (b) Kanisa lililoko Laodika (Ufunuo 3:1417)

12. Ni kiasi gani ambacho Wakristo wa mwanzo walivutiwa na mafundisho ya mitume, ushirika, kumega mkate, na maombi? (Matendo ya Mitume 2:42) …………………………………………………………………….. ………………………………………………………………………… …………………………………………………………………………

13. Ninapaswa kujihadhari na nini iwapo nintaka kumpendeza Bwana? (Waebrania 10:25) …………………………………………………….

……………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………

14. Baadhi ya sababu ambazo zitafanya nijiunge na kanisa ni: ……………..

……………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………

Kwa imani yako, umeungana na Yesu Kristo na, katika hali ya kiroho, pia umeungana na Wakristo wote halisi. Sasa inakupasa kufikiria juu ya utaratibu rasmi wa hatua ya kujiunga na kanisa. Ushirika huu ni muhimu sana na kazi yake ni kubwa sana hivi kwamba Wakristo wanahitaji kuungana kwa kila njia iwezekanayo. Kwa msaada wa kanisa na mchungaji wako, utaendelea kukua katika Kristo.

Pongezi kwa kumalisa masomo haya. Siku zaidi za furaha ziko mbele yako, unapoendelea kwa ujasiri kumtumikia Mungu!

**Mstari wa Kumbukumbu**

Wala tusiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi ya wengine, bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia. (Waebrania 10:25)

***Cheti hiki Kimetunukiwa***

________________________________________________________

*Baada ya Kumaliza*

# ***"Masomo ya Msingi ya Biblia"***

________________________________________________________

Kanisa ________________________________________________

Mshauri ________________________________________________

Mchungaji ______________________________________________

Tarehe __________________________________________________

## MWONGOZO WA KIROHO

Njia ya WOKOVU…………….... II Wakorintho 5:17, Matendo ya Mitume 4:12, Yohana 14:6, Matendo ya Mitume 16:31, Warumi 10:9

Faraja wakati wa UPWEKE…....... Zaburi 23, Isaya 41:10, Waebrania 13:5, 6

Faraja wakati wa HUZUNI ………... II Wakorintho 1:3-5, Warumi 8:26-28

Kutulizwa wakati wa MATESO……… II Wakorintho 12:8-10, Waebrania 12:3-13

Mwongozo wakati wa UAMUZI ………. Yakobo 1:5-6, Mithali 3:5-6

Ujasiri wakati wa HOFU…………… Waebrania 13:5-6, Waefeso 6:10-18

Amani wakati wa MSUKOSUKO …………… Isaya 26:3-4, Wafilipi 4:6-7

Pumziko wakata wa UCHOVU ………….. Mathayo 11:28-29, Zaburi 23

Nguvu wakati wa MAJARIBU…………… Waebrania 4:15, Yakobo 1:12-16, 1 Wakorintho 10:6-13

Onyo wakati wa KUTOJALI ……… Wagalatia 5:19-21, Waebrania 26-31

Msamaha wakati wa KUHUKUMIKA ……….. Isaya 1:18, 1 Yohana 1:7-9

## VIWANGO VYA KIROHO

Amri Kumi…………………………..Kutoka 20:17
Mahubiri mlimani ………………….. Mathayo 5-7
Kanuni ya thamani …………………. Mathayo 7:12
Amri kuu …………………………… Mathayo 22:36-40
Agizo kuu…………………………… Mathayo 28:18-20
Haki ya Imani ……………………….Warumi 3:19-28
Sheria ya Kifalme…………………… Yakobo 2:8, Warumi 13:8-10
Amri mpya ya Kristo ……………….. Yohana 13:34-35
Upendo wa Kikristo …………………. 1 Wakorintho 13